

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5  
Fax No. +255 026 2322624  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA.**

## **TAARIFA KWA UMMA**

Mkutano wa 19 wa Bunge la Kumi na Moja ambao ni mahsusni kwa ajili ya kupitisha Bajeti ya Serikali utanza Jumanne Tarehe 31 Machi 2020 na kuendelea hadi tarehe 30 Juni 2020.

Kufuatia janga la ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya Corona utaratibu wa undeshaji wa Shughuli za Bunge katika Mkutano huu utakuwa tofauti na ilivyozoeleka. Kwa mujibu wa Spika wa Bunge, Mhe. Job Ndugai (Mb), mabadiliko yafuatayo yatafanyika ikiwa ni hatua za kujikinga na ugonjwa wa Corona wakati wa vikao vya Bunge.

**Mosi**, muda wa vikao vya Bunge utapunguzwa kutoka saa tisa kwa siku hadi saa nne ambapo; vikao vitakuwa vikifanyika kuanzia saa 8:00 Mchana hadi 12:00 Jioni. Hata hivyo mabadiliko ya muda hayatahusu kikao cha kwanza ambacho kilishapangwa toka awali kuanza saa tatu.

**Pili**, idadi ya Wabunge watakaoingia Bungeni imepunguzwa ambapo katika Mkutano huu; Wabunge watakaokuwa wanaingia ndani ya Ukumbi wa Bunge hawatazidi mia na hamsini (150) kwa wakati mmoja. Wabunge watakaoingia Bungeni ni wafuatao;

- Mhe. Spika;
- Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni;
- Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni;
- Wanadhimu wa kila Chama;
- Mawaziri na Naibu Mawaziri;
- Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Mawaziri Vivuli na Manaibu wao;
- Wajumbe wa Kamati ya Uongozi;
- Wajumbe wa Tume ya Bunge;
- Kamati ya Bajeti; na
- Makamu Wenyeviti wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge ambao hawataingia ndani ya Ukumbi wa Bunge, watafuatilia Shughuli za Bunge kupitia Runinga katika Kumbi na maeneo mengine yaliyopangwa.

**Tatu**, kufuatia utaratibu huu mpya Waheshimiwa Wabunge watauliza Maswali na kujibiwa kwa njia ya maandishi kupitia *Tablet* zao. Katika utaratibu huu Wabunge wote watafumiwa Maswali na Majibu, na Mbunge mwenye Swali la Msingi atarahusiwa kuuliza Maswali ya Nyongeza kwa njia ya maandishi kupitia *Tablet*. Vilevile hakutakuwa na kipindi cha Maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

**Nne**, Kuhusu utaratibu wa upigaji kura wakati wa kupitisha Bajeti za Wizara Waheshimiwa Wabunge watapiga kura kwa njia ya mtandao kupitia *Tablet* zao isipokuwa wakati wa upitishaji wa Bajeti kuu ya Serikali ambapo Wabunge wote watapata fursa ya kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja. Pamoja na hayo Waheshimiwa Wabunge watakuwa pia na uwezo wakuchangia katika mijadala ya Bajeti, Miswada na Maazimio kwa njia ya maandishi kupitia *Tablet* zao.

Kwa mujibu Mhe. Spika mabadiliko haya ni ya muda kufuatia ugojwa wa Corona. Hivyo mabadiliko mengine yanaweza kufanyika au haya yakaondolewa kwa kuzingatia hali itakavyokuwa.

Ratiba yote ya Mkutano wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz).

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,  
Ofisi ya Bunge,  
**DODOMA.**

30 Machi, 2020.